

# Ukweli wa Injili

MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA  
KAZI YA KIMISHENI ULMWENGUNI KOTE

## MFARISAYO NA MTOZA USHURU

*Habari ifuatayo ni ya hadithi ya mfano ambaa Yesu alitoa katika (Luka 18:9).*

### MAELEZO:

Mafarisayo walikuwa moja ya kikundi kikubwa sana cha kidini katika jamii ya Wayahudi. Ni kundi ambalo lilikuwa tajiri sana. Washirika wake walishika sana sheria nyngi za Musa, na hata walionelea kwamba iliwabidi kufuata hata tamaduni zilizotokana na mafundisho ya Musa, tamaduni ambazo zilikuwa zimepitishwa toka kwa vizazi tofauti kwa njia ya mdomo. Neno Farisayo lilimaanisha *aliyetengwa*. Mafarisayo walijitenga kutokana na uchafu ulioletwa na ibada za Wayahudi, wakajitenga huku wakijifanya kundi takatifu lisilo na dosari. Wao walifuata miongozo ya kundi lao, na wakajihisi kwamba walikuwa wenye haki kwa sababu ya ufuataji wao wa sheria. Hata ingawa hapo mwanzoni Mafarisayo walikuwa wamekubalika mbele za Mungu, mwishowe wengi wao walipoteza ile roho na kusudi la kuweko kwa sheria kwa maana walianza kutilia mkazo usafi wa nje badala ya usafi wa moyo. Ibada zao nazozikawa ndefu na za kujionyesha, kwa sababu walitaka kuonekana na wanadamu. Basi maisha yao yakaonekana kuwa na aina ya uungu, lakini wengi wao wakaanza kuwa na kiburi na maringo ya utakatifu wa kibinafsi, huku wakiwadharau

watu wale wengine.

Watoza ushuru nao walikuwa watu wa kawaida. Angalau wao walikuwa ni Wayahudi ambaa walifanya kazi serikali ya Kirumi, watawala wa Wayahudi. Watu hawa



walidhihakiwa na wananchi wenzao kwa sababu walionekana kama wasaliti, kwa maana walikusanya ushuru kumfaidi mgandamizaji wa Wayahudi. Wakati mwingi watoza ushuru hao walikuwa watu wanaopenda rushwa sana, na pia walikuwa watu wasiokuwa na ukweli kazini mwao (kazi ya ukusanyaji ushuru).

### MFANO WA MFARISAYO NA MTOZA USHURU:

Mafarisayo aliingia kwa ujasiri mle hekaluni. Mavazi yake marefu yalitoa mlio wa mkwaruzono yalipoguzana na mtoza ushuru ambaye alikuwa akiingia hekaluni kuomba,

huku kichwa chake kikiwa kimeinamishwa chini kwa unyenyekevu. Mfarisayo akamtazama mtoza ushuru huyo kwa mtazamo wa dharau huku akimuondokea wasiguzane ili asitiwe dosari na kuwepo kwa mtu huyo mwenye dhambi.

Huku akisimama kando akiwa amejitenga Mfarisayo huyo akainua mikono yake kwa ibada, macho yake yakatazama juu kuelekezwa mbinguni, nayo sauti yake ikasikika kote mle hekaluni ikiomba:

*“Mungu! Asante kwa maana mimi si kama watu wale wengine—watu wa kukula hongo, wasio na ukweli, wachafu, na wasinzi! Asante Mungu kwa sababu mimi si o kama huyu mtoza ushuru. Kila wiki nafunga mara mbili na ninatoa fungu la kumi kwa kila nilicho nacho.”*

Mfarisayo akaendelea na maombi kwa kumtambua Mungu na kutoa shukrani zake. Lakini pia akaendelea kutukiza sifa zake na utakatifu wake wa kibinafsi. Nako huko mbali kwenye upande mmoja wa hekaluni mtoza ushuru alikaza macho yake sakafuni, akawa na masumbu na majonzi mengi kwa sababu ya dhambi zake. Na kama ilivyokuwa desturi ya watu wa nyakati hizo za kujieleza wakati mtu anapopatwa na majonzi mengi, mtoza ushuru alipigapiga kifua chake. Sauti yake ikasikika ikiwa kama ya mtu anayetaka

*(Inaendelea kutoka ukurasa 2)*

# MAMBO AMBAYO BIBLIA

## Inafundisha Kuhusu...

### Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

### Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, I Yoh. 4:7-21

### Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

### Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1,

5-6

### Uhuru Kutokana na Dhambi

I Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

### Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

### Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, I Pet. 1:15-16,

Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

### Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

### Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, I Kor. 12:12-13, Kol.

1:18

### Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

### Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,

Yn. 13:14-17

### Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

### Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor.

7:10-11

### Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

### Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt.

25:31-46

### Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

### Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

### Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Endelea kutoka ukurasa I)

kutokwa na machozi kutokana na uchungu wa moyo wake, hata ikawa vigumu kusikia maombi aliyokuwa akifanya:

“Ee Mungu nirehemu, kwa sababu mimi ni mwenye dhambi.”

### SOMO:

Yesu alitoa mfano huo kwa wale amba walikuwa na imani na utakatifu wao wa kibinagsi na kuwadhihaki watu wale wengine. Akasema, “Nawaambia, huyu alishuka kwenda nyumbani kwake amehesabiwa haki kuliko yule; kwa maana kila ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhiliye atakwezwa”

Mfarisayo huyo alikuwa na udini mwingu ndani yake na alifuata kanuni bora nyingi, lakini moyo wake ulikuwa na kiburi. Yeye alikuwa na utakatifu wa kibinagsi na akajiona kwamba alikuwa wa kiroho zaidi ya watu wale wengine. Lakini kazi zake nzuri na sadaka zake kwa Mungu hazingewza kumwokoa. Lakini yule mtoza ushuru kwa moyo wake wa unyenyekevu alimwomba Mungu ili amurehemu. Kwa kweli yeye ndiye alisamehewa dhambi zake na siku hiyo hiyo akaupata wokovu.

Wokovu ni kipawa kutoka kwa Mungu kwa wale amba watanyenyekea na kukiri kwamba wao ni wenye dhambi wenye hitaji la Mwokozi. Tabia nzuri, dini, na matendo mema hazimfanyi mtu kuhesabiwa kuwa mwenye haki. Kanisa la siku zetu limeitwa ili kujitenga na dhambi ya dunia. Ni kweli kwamba kila mtoto wa Mungu ametengwa na ulimwengu na basi kila mmoja anatakiwa kuishi kwa moyo wa unyenyekevu na kuepuka roho ya Mafarisayo ya mtu kujiona kuwa na utakatifu wa kibinagsi. Utakatifu wote wa kweli unatoka kwa Bwana wetu, sio kwa mtu binagsi.

—mws

### UKWELI WA INJILI

Gazeti la ‘Ukweli wa Injili’ huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia amba umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaotetwa na utakaso wa Yesu Kristo; amba hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamiletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinagsi na wa upendo amba msingi wake ni ukweli. Waandishi: Michael na René Smith

### UAGIZAJI

*Ukweli wa Injili* ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka jinsi mungu anavyotuongoza. Tutembeleesi katika tovuti yetu ya [www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org) ili uagize jalida hili kupitia kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine amba wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la *Ukweli wa Injili*.

### WASILIANA NASI

Gazeti a *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimishenari ambazo sisi hufanya huwezekana kupitia kwa matoleo ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

Ukweli wa Injili, 605 Bishops Ct., Nixa, MO 65714 USA  
[editor@thegospeltruth.org](mailto:editor@thegospeltruth.org)

# Tahariri



*Ee mwanadamu, yeye amekuonyesha yaliyo mema; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako? – Mika 6:8*

Tunalo deni kwa Mwokozi wetu ambalo kamwe hatutaweza kulilipa. Sisi hatukustahili wala hatukuwa na haki ya kupokea neema na upendo wake. Lakini

Yeye alitusame dhambi zetu. Kuna mafundisho mengi muhimu katika Maandiko lakini unyenyekevu ni moja ya mafundisho makuu katika Biblia. Mungu anataka kila mtoto wake kwenenda kwa njia za unyenyekevu na upendo. Ni jambo la huzuni kubwa kuona kiburi cha kiroho kikidhihirika maishani mwa watu ambaao wanajua ukweli mwingu.

Mzigo mbao Mungu ameweka moyoni mwangu katika robo hii ya mwaka ni kuhusu utakatifu wa kibinagsi. Hata ingawa somo hili ni tofauti na ukweli mwinguine wa kithiolojia ambaao tulijifunza katika robo zingine za mwaka, hili ni somo muhimu kabisa kama hizo zingine.

Tunaweza kuwa tunajua ukweli mwingu na mafundisho mengi ya Kikristo; lakini ikiwa tutakuwa na kiburi cha kiroho, na kama tutatumaini kazi zetu wenywewe, basi tutakosa baraka za kweli za Ufalme wa Mungu katika maisha haya na maisha yajayo.

Mimi ninakumbuka kama nikiwa kijana mdogo niliona kundi la watu ambaao walianza kutukuza utakatifu wao wenywewe. Kwa kweli wao walikuwa watu wazuri kwa nyanja mbalimbali, lakini wao wakapatwa na roho ya kuwa na ukali wa kuwatoa watu wale wengine makosa. Walianza kuwa na utakatifu machoni pao wenywewe na kuanza kusema kwamba mienendo yao ndio njia ya mtu kumfikia Baba. Mimi namkumbuka baba yangu (mzazi) akiniambia kwamba ikiwa sisi tutautenganisha ukweli na upendo, basi tutakuwa tumepotea kabisa. Ni jambo muhimu kwa mtoto wa Mungu kuenenda kwa njia za upendo na unyenyekevu. Kamwe hatutaweza kustahili kupata baraka za Mungu na pia hatutawahi kuwa “wazuri kwa viwango vya kutosha” kwa kutumia nguvu zetu wenywewe.

Kila siku mimi nategemea rehema na msaada wa Mungu ili kuniwezesha kuishi maisha ya utakatifu. Shauku letu kubwa maishani linastahili kuwa ni kuzaa matunda mema na kuwa na shauku la kutenda mambo mema. Lakini matendo hayo sio yanayofanya mtu kustahili wokovu, mbali yao ni ushuhuda kwamba Kristo anaishi ndani mwetu.

Maneno yetu, mahubiri yetu, maisha yetu, na roho wetu wa ndani – yote hayo yanahitaji kuwa katika hali ambayo Kristo atawea kutukuzwa. Baadhi ya watu ambaao ni vigumu sana kuishi nao ni wale ambaao wanategema kazi na mawazo yao na ambaao wana kiburi na maringo ya kiroho. Hawa ni watu ambaao hawataomba msamaha hata ingawa wametenda mambo yasiyolingana na tabia njeama za kiroho. Utakatifu wa kibinasi ni chukizo kubwa kwa Mungu na matokeo yake ni kwamba watu wanakuwa na misimamo mikali, au kuanza kujiingiza kwa mambo ya kidunia.

Hebu basi Kristo ainuliwe maishani mwetu na katika mwili wa Kristo. Sisi hatuna wokovu au neema ya kuwapatia wanadamu kwa nguvu zetu wenywewe, lakini tunaweza kuwaelekeza wanadamu kwake Yeye ambaye alitufia. Tunaomba kwamba ulimwengu huu utamwona Kristo na kwamba Yeye ndiye ambaye ataonekana katika jukwaa la maisha yetu, kwani Yeye ndiye mwanzilishi na mkamilishi wa imani yetu.

Michael W. Smith

Julai 2015



*Tutembelee kwa*

[www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org)

*ili uagize na kusoma*

*jarida letu.*



## Hayo Imewapasa Kuyafanya...

(Mathayo 23:23-24; Luka 11:42)

Wakati mwingu Yesu aliwakaripia Mafarisayo ambao walikuwa na utakatifu wa kibinafsi. Kwa kweli Yeye hakupuuza jinsi Mafarisayo walikuwa watu waangalifu kwa mambo yao, wala hakudharau jinsi walivyoshughulikia kwa umakini mwingu maswala ya sheria; lakini Yeye aliwakemea kwa sababu wao hawakutilia maanani mambo ambayo ni muhimu zaidi—kufanya haki, kuwahurumia watu, kuwa na imani, na mtu kumpenda Mungu wake.

“Hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache.”

Kama ilivyo kwa watu wa siku hizi wanaojifanya kuwa na utakatifu wa kibinafsi, Mafarisayo walikuwa na bidii kubwa kutilia maanani mambo fulani, lakini wakati mwingu maisha yao yalidhihirisha roho ya kimwilli, roho ambayo ina upungufu mwingu wa upendo kwa watu wale wengine.

Kuna watu wanaosema kwamba wanayo imani hivi kwamba hawana haja ya kunywa madawa wala kutibiwa na madaktari. Nao wengine hujihesabia haki kutokana na mavazi ya kiwango cha wastani ambayo wao hupendelea kuvaai. Wengine hata hujihesabia haki kutokana na matoleo yao na jinsi wanavyowasaidia watu. Lakini baadhi ya watu kama hawa huwa na upungufu mwingu wa upendo na unyenyekevu wa Kristo.

Basi wewe mtu wa Mungu tunakuomba uendelee kuwa mtu mtifui na mtu mwangalifu kwa mambo ambayo yanaonekana na wanadamu, lakini pia usiache kuzingatia mambo ya kiroho ambayo ni muhimu zaidi.

# MWONGOZO WA KUJIFUNZA BIBLIA

## SOMO: UTAKATIFU WA KIBINAFSI

**Somo la Biblia:** *Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.* –Waefeso 2:8-9

**Muhstasari:** Utakatifu wa kibinafsi ni jambo ambalo ni kinyume na ujumbe wa Injili na ni jambo ambalo humletea mtu mauti kwa mambo ya kiroho. Wokovu si kitu ambacho mtu anaweza kupata kama malipo ya bidii zake, mbali ni kipawa kutoka kwa Mungu. Daima utukufu wote unastahili kupewa Baba yetu. Haistahili kamwe mtu kujipatia utukufu huo au kuupatia kikundi chochote cha wanadamu.

### I. SIFA ZA WATU WALIO NA UTAKATIFU WA KIBINAFSI

- A. Luka 10:29 Wanajihesabia haki mbele ya wanadamu wenzao.
- B. Mathayo 23:27-28 Kwa nje huonekana watakatifu lakini kwa ndani wamejaa uovu.
- C. Mathayo 6:1-2 Wanapenda kuonekana na wanadamu wenzao.
- D. Warumi 10:1-3 Wanategemeza utakatifu wa kibinafsi.
- E. Mathayo 7:3-5 Huwa na haraka ya kuonyesha upungufu wa watu wale wengine.
- F. Luka 7:39 Angalau wanawahukumu watu wale wengine.
- G. Isaya 65:5, Luka 18:9 Hujitokuza wao wenyewewe na kudharau watu wale wengine.
- H. Mithali 20:6 Wao hutangaza jinsi walivyo wazuri.
- I. Mithali 30:12 Machoni mwao wao hujiona kuwa safi.

### II. UTAKATIFU WETU WA KIBINAFSI

- A. Luka 11:42-44 Ni wa nje.
- B. Isaya 64:6 Ni kama nguo chafu.
- C. Isaya 57:12 Hauna faida yoyote.
- D. Luka 16:15 Ni chukizo kwa Mungu.

E. Ufunuo 3:16-17 Hupofusha.

F. Mathayo 5:20 Utatufanya kutofika mbinguni.

### III. UTAKATIFU WA KWELI NA KUHESABIWA HAKI

- A. Waefeso 2:8-9 Hautokani na sisi mbali ni kwa neema.
- B. Wagalatia 2:16 Hautokani na sheria mbali ni kwa imani.
- C. Tito 3:5 Hautokani na kazi zetu mbali ni kwa rehema.

### IV. ANAYESTAHILI UTUKUFU

- A. Isaya 42:8 Mungu hatoshiriki utukufu wake.
- B. Danieli 4:28-31 Mfano wa Nebukadneza.
- C. 2 Wakorintho 10:17-18 Kujitokuza katika Bwana.
- D. Mathayo 5:16 Kutenda matendo ya kumtukuza Baba.

### TAMATI:

*Kila njia ya mtu ni sawa machoni pake mwenywewe; kutenda haki na hukumu humpendeza Bwana kuliko kutoa sadaka. Macho yenye kiburi, na moyo wa kutakabari, hata ukulima wa waovu, ni dhambi.* – Mithali 21:2-4

# UTAKATIFU WA KIBINAFSI

*Nakala ya kuandamana na mafunzo ya Biblia*

## WOKOVU NI KIPAWA KUTOKA KWA MUNGU

Wokovu ni ujuzi wa mtu kujua wema wa kiungu amba Mungu huwapatia wale amba hunyenyekia mbele zake na kutubu dhambi zao. Mtu hapati wokovu kwa nguvu zake, au uvumilivu wake, au uweza wake; wokovu ni kazi ya kimuujiza ya Mungu. Maandiko yanaonya kwamba wokovu “si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu” (Waefeso 2:9). Utakatifu wa kibinafsi ni ile hali ya mtu kuamini wema wake mwenyewe, kuamini maoni na matendo yake huku akiona kwamba watu wale wengine wamepotea. Kuna wengi amba wametenda dhambi ya kujifanya utakatifu wa kibinafsi. Mtoto wa Mungu ambaye ana utakatifu wa kibinafsi ni yule ambaye anaamini wema na matendo yake mwenyewe, huku akijaribu kutumia mambo hayo yawe msingi wa kuhesabiwa haki na Mungu. Yesu alitumia wakati mwangi hapa duniani hudumani mwake kushughulikia swala la watu amba walikuwa na kiburi cha kiroho na utakatifu wa kibinafsi. Ndiposa akawaonya watu, “Jilindeni na chachu ya Mafarisayo.” Chachu hiyo ni unafiki, ni utakatifu wa kibinafsi, ni upotovu wa mtu kujifikiria jinsi alivyo na uwezo na cheo cha hali ya juu.

## UTAKATIFU NI JAMBO LINAWEZKANA TU KUPITIA KWA KRISTO NA ROHO WAKE

Watu wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu, hii ndiyo sababu wanahitaji Mwokozi. Ni kwa kupitia kwa Kristo tu ndio ambavyo mwanadamu anaweza kuishi maisha matakatifu. Basi utukufu na heshima zote zinahitaji kumwendea Baba, na hakuna nafasi kwa kiburi cha mtu kujitokuza kwa mambo ya kiroho. Mtume Paulo alisema, “Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu...” (Wagalatia 2:20). Neema zote na uweza wa mtu kuishi kama anavyotakiwa na Mungu ni mambo ambayo yanawezekana tu kutokana na kazi za Kristo na kutokana na Roho wake anayeishi ndani yetu. Basi nguvu za Mungu ndilo jambo ambalo linastahili kutiliwa umuhimu na ndilo jambo la kutegemewa, sio uwezo hafifu wa mwanadamu.


## ISHARA ZA MTU ALIYE ROHO YA UTAKATIFU WA KIBINAFSI

Watu wenye utakatifu wa kibinafsi huwa na tabia ambazo zinatambulika katika Maandiko. Ni wajibu wa mtoto wa Mungu kuitambua dhambi hii ili ajue inapojitokeza. Watu wenye utakatifu wa kibinafsi huwa na tabia za wao kujihesabia haki (Luka 10:29), hata wakati ambapo maisha yao hayafikii viwango vinavyofundishwa katika Biblia. Kama inavyoonekana katika maisha ya Mafarisayo watu hawa huonekana kufuata amri kadha wa kadha kwa dhati kwa mambo yanayoonekana na wanadamu ili wao waonekane kuwa watakatifu. Hii ndio sababu Yesu alisema

watu hawa huonekana kuwa watakatifu kwa nje, lakini ndani yao kulijaa unafiki na dhambi (Mathayo 23:27-28). Wao hupenda kutukuzwa na kuonekana kuwa mabingwa kwa mambo ya kiroho (Mathayo 6:1-2).

## KUUTHIBITI UTAKATIFU WA KIBINAFSI

Mtume Paulo alinena kuhusu watu wale amba “wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu” (Warumi 10:3). Watu wenyewe utakatifu wa kibinafsi huruhusu maoni na njia zao kuwa muhimu kuliko mafundisho rahisi



ya Neno la Mungu. Wao huwa na haraka ya kutangaza wema wao (Mithali 20:6) na hujiona safi machoni pao wenyewe (Mithali 30:12), ilhali wakati huo huo roho zao huwa zimejaa uchafu na kiburi. Wanatangaza na kuonekana kuwa watakatifu (Isaya 65:5) lakini kazi zao huwa hazikubaliki machoni pa Mungu.

Watu wenyewe utakatifu wa kibinafsi huwa na haraka ya kuwahukumu watu wale wengine na kuwapata kuwa na hatia (Luka 6:41). Mathayo 7:3 inasema, “Basi, mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii?”

## UTAKATIFU WA MWANADAMU NI WA NJE TU

Utakatifu wa Mungu ukiwa ndani ya mtu unamwongoza kuwa na utakatifu au usafi wa nje amba huandamana na roho yenye unyenyeketu na upendo. Utakatifu wa mwanadamu ni wa nje (Luka 11:42-44) na huwa kama nguo iliyotiwa unajisi (Isaya 64:6). Mwanadamu hana utakatifu wake wa kibinafsi na hana nguvu za kubadilisha hali halisi ya moyo wake bila nguvu za Mungu. Utakatifu wote wa mwanadamu hautamfaidi kitu (Isaya 57:12).

*(Inaendelea kutoka ukurasa 6)*



(Endelea kutoka ukurasa 5)

Mtu kutenda mambo mema ni jambo la manufaa lakini ikiwa kama msukumo wa kufanya mambo hayo hautokani na Mungu aliye ndani yake, basi matendo hayo yote huwa hayana faida kwa maswala ya uzima wa milele.

#### **WATU WENYE UTAKATIFU WA KIBINAFSI HAWATAINGIA MBINGUNI**

Utakatifu wa mtu binafsi humfanya kuwa kipofu, na hufanya watu kujihadaa kwamba wako salama kwa mambo ya kiroho: "Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi." Kusanyiko la Laodikia walijiona kwamba wametosheleka na kwamba walikuwa matajiri kwa mambo ya kiroho; lakini bila upendo kamili kwa Mungu wao walikuwa maskini, uchi na vipovu katika utakatifu wao wa kibinasi. Zaidi ya hayo wao walikuwa wameacha kumtegemea Mungu na kuanza kutagemea matendo yao mazuri ya kidini. Lakini utakatifu wa kibinafsi ni dhambi na ni jambo litakalomzia mtu kufika mbinguni. Hii ndio sababu Yesu alisema, "Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni" (Mathayo 5:20).

#### **AINA YA UNGU**

Mafarisayo walikuwa na aina ya ungu. Wao waliomba, walijinyima chakula, walitoa zaka zao, n.k. lakini pia walitegemea kuhitimu kwoo kwa njia ya utakatifu wa kibinafsi badala ya kutegemea neema ya ukombozi wa Mungu. Wagalatia 2:16 inasema, "mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; . . . maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki." Mwanadamu anaweza kufuata mafundisho mengi ya Neno la Mungu na kuvala mavazi ya kiwango cha wastani. Anaweza pia kupeana pesa zake kwa ukalimu na awe mtu mwenye sala nydingi. Pia anaweza kuwa mwaminifu kwa ibada za kanisa, lakini akose kufika mbingu

kwa sababu ndani yake kumekosekana roho ya upendo, roho ya unyenyekevu, na roho ya kutegemea utakatifu wa Kristo pekee. Hata ingawa viwango vya maisha na ufuataji wa sheria ni mambo muhimu, utakatifu wa kweli huanza moyoni mwa mtu.

#### **NI MAMBO GANI WEWE UNATILIA UMUHIMU?**

Utakatifu wa kibinafsi hutukuza nafsi ya mtu badala ya kumtazama Mwenyezi Mungu. Lakini Mungu kamwe hatoshiriki utakatifu wake na mtu mwingine (Isaya 42:8). Wanadamu wanapoacha kumpatia Mungu utukufu hapo hapo utukufu unakoma kuonekana. Kipimo cha utukufu ulio na kundi fulani la Wakristo hakionekani kulingana na jinsi kikundi hicho kinawea kuimba kwa sauti nzuri ama jinsi kinawea kuvala mavazi yanayofaa. Utukufu ni upako wa Mungu wa kila siku ambaa huleta amani, furaha, nguvu, upendo, na unyenyekevu. Wakorintho wa Pili 10:17-18 inasema, "Lakini, Yeye ajisifuye, na ajisifu katika Bwana maana mtu mwenye kukubaliwa si yeye ajisifuye, bali yeye asifiwaye na Bwana." Lengo la matendo mema ambayo mtoto wa Mungu hufanya yanahitaji kuwa ni kumtakuza Baba aliye Mbinguni (Mathayo 5:16).

Basi wewe hebu kuwa macho dhidi ya chachu ya Mafarisayo. Utakatifu wa kibinafsi unaweza kumwingia mtu au kikundi cha watu "Basi Bwana tusaidie kuishi kwa unyenyekevu, huku tukiwa kwamba hatutumaini kazi zetu za utakatifu, lakini tutegemee tu damu ya Yesu Kristo ambayo inafaa sana. Amina."

-mws

# MASWALI na MAJIBU

## BASI UMUHIMU WA MATENDO MEMA NI UPI KAMA MATENDO HAYO HAYATUOKOI?

'Waefeso 2:8-9 ni andiko muhimu ambalo hunukuliwa mara nydingi: "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."

Wokovu ni kazi ya kiungu inayofanywa na Mungu katika moyo wa mwanadamu na mtu hawezi kuustahili au kuufanya kazi wokovu huo. Huu ni ukweli wa ajabu lakini watu wengi hawatilii mkazo aya ya 10 ambayo imefuata aya hizo za hapo mbele: "Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo."

Kuna watu wengi wanaojiita Wakristo na wanaosema kwamba neema ya wokovu wa Mungu imo maishani mwao lakini kazi zao, tabia zao, na mielekeo yao maishani haijabadilika. Badala yake neema inatumiwa kufunika au kujisingizia matendo yao maovu ama matendo ya wao kutotii Neno la Mungu. Sisi hatuokolewi kwa matendo lakini tumeumbwa upya ili tutende mema na kuishi maisha ya wema: "... kama mlivyovitoa viungo vyenu vitumiwe na uchafu na uasi mpate kuasi, vivyo hivyo sasa vitoeni viungo vyenu vitumiwe na haki mpate kutakaswa" (Warumi 6:19).

Yesu alitwambia kwamba tutawajua watu kulingana na matunda au matendo yao (Mathayo 7:16-17). Mara nydingi moyo wa mtu hujulikana kutokana na matendo yake. Nayo miyo haifanywi kuwa mitakatifu kwa njia ya kufunga, kuomba, kutoa, kujinyima, kuishi maisha yenye viwango ambavyo vinafaa vya kiasi, kuhudhuria kanisa, ama utumishi n.k.; lakini ikiwa mtu ameokolewa kwa neema ya Mungu matendo mema yatakuwa ndio tunda la moyo wake ambao ni mtakatifu.

Biblia inatoa miongozo mingi ya jinsi watu wa Mungu wanahitaji kuishi na kutenda kama watu watakatifu wa Mungu. Wao wanahitaji kutengwa na kutofautishwa na ulimwengu wenye dhambi, sio tu kwa mielekeo ya maisha yao, wala kwa jinsi wanavyojitolea, mbali hata pia kwa mavazi ambayo wanavaa na mambo ambayo wanashiriki maishani.

Tuliumbwa  
Tutende  
Matendo  
Mema



Yesu akasema, "Mtu akinipenda, atalishika neno langu; ... Mtu asiyenipenda, ye ye hayashiki maneno yangu" (Yohana 14:23-24). Mtu mtiifu huzaa matendo mema. Matendo mema hayamwokoi mtu, lakini ukosefu wa matendo mema unaweza kufanya mtu kupoteza wokovu wake.

Kitabu cha Yakobo kinafundisha kwa uwazi kabisa kwamba imani isiyo na matendo imekufa. Imani iliyo hai au mtu kuamini Mungu ni jambo ambalo litazaa mtendo matakatifu na yenye faida. Ukosefu wa matendo mema ni ishara ya upendo ambao umekufa na imani iliyo utupu na isiyo na kitu ndani yake. Yesu

alikuja ili kuwaokoa wanadamu kutokana na dhambi zote, ili Wakristo wawe watu spesheli wenye tamaa ya kufanya mema (Tito 2:11-14).

Ni jambo la ajabu sana ikiwa mtu ataishi maisha ya kuzaa matunda mema na kufanya matendo ambayo yanatokana na tabia nzuri za utakatifu. Matendo hayo mazuri huwa hayamwokoi mwanadamu, lakini yanamsaidia kudumisha na kukuza ujuzi wake ndani ya Mungu.

## TUSEME NINI KUHUSU MAKANISA WANAOSEMA KWAMBA WAO NDIO NJIA YA PEKEE YA WOKOVU?

Yesu alisema, "Mimi ndimi mlango; mtu akiingia kwa mimi, ataokoka" (Yohana 10:9). Hakuna mtu, kanisa, au kundi la wahubiri ambao wanaweza kumpatia mwanadamu wokovu. Hakuna utaratibu ambao mtu anaweza kufuata ili astahili wokovu ama kuufanya kazi. Wokovu ni kipawa kutoka kwa Mungu kinachopitia kwa Mwana wake wa pekee.

Kanisa fulani likijitokuza kwamba wao ndio njia ya kufika mbinguni basi hicho ndicho kilele cha kiburi cha kiroho na kilele cha utakatifu wa kibinafsi. Washiriki wa kanisa ni watu ambao wameitwa na Mungu na kuokolewa kutoka dhambini. Ujumbe wa Kanisa ni ujumbe wa kuongoza watu hadi hapo msalabani ili wapate imani ambayo msingi wake ni Neno la Mungu. Mhudumu yeyote wa Injili ama kundi la watu ambao wanafundisha wokovu unaotokana na matendo ya mtu au wanafundisha kwamba ni lazima watu wapitie kanisani mwao ili wawze kukutana na Mungu basi hilo ni tendo la kuharibu injili safi ya Kristo. Jambo hilo pia liko tofauti na ukweli ambao tumejifunza. Wanaofudisha mambo kama hayo wamepotoka na Wakristo wanahitaji kuepuka watu kama hao (Warumi 16:17).

-mws



**JE, WAJUA?**

*Kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi. – Isaya 64:6*

Mungu aliona wana wa Israeli kuwa watu wachafu ambao walikuwa wamenajisika hata ingawa wao walikuwa waombaji sana, walikuwa watu wa kutoa kafara na sadaka, watu ambao hata walipenda kumsifu. Yeye alichukizwa na ibada zao kwa sababu zilijaa uharibifu.

Utakatifu wao ulikuwa kama matambara machafu. Aliyaona matendo yao ya utauwa kama ambayo yalijaa uchafu. Katika lugha ya Kiebrania maana halisi ya neno “matambara machafu” ni “kitambaa ambacho tayari kilishatumika na mwanamke wakati wa hedhi yake.”



**Hubiri Ujumbe Ambao Mimi Nimekupatia**

### Anwani

The Gospel Truth  
605 Bishops Ct.  
Nixa, MO 65714  
USA  
Email:  
[editor@thegospeltruth.org](mailto:editor@thegospeltruth.org)

### UTAKATIFU KWA BWANA

*Ondoka, uende Ninawi, mji ule mkubwa; ukaihubiri habari nitakayokuamuru. – Yona 3:2*

Mungu alimpatia nabii Yona kazi ya kwenda Ninevi “ukaihubiri habari nitakayokuamuru.” Huenda manabii wengine hawatafurahishwa na mahubiri yako, pengine jamii yako haitapenda ujumbe wako, na huenda hata watu wasitambue jinsi ulivyojitlea kazini mwa Mungu. Hata pengine watu watakuufuza na kukulazimisha kutoroka kutoka kwenu, lakini wewe endelea kuwa mwaminifu. Kamwe usihubiri maoni ama mawazo yako, lakini uhubiri kile ambacho Roho ananena kwa njia ya upendo, hekima, na ujasiri utokao kwa Roho Mtakatifu.



Sio wajibu wa mahubiri ya Injili kumfurahisha Mkristo. Hata ingawa kutakuwa na nyakati za kuhubiri faraja na kuwashimiza wasikilizaji wako, Wakristo huweza kukua kutohana na kufanya bidii katika Ukristo wao na wakati wahubiri wao wanawafanya kutokuwa na utulivu maishani. Je, Wakristo watakuua vipi ukweli ikiwa mahubiri ya Injili haitangaza kila ambacho Roho amesema?

Shetani atajaribu kumnyamazisha kila mhuduma wa kweli wa Mungu. Ukihubiri hili mtu yule atakasirika. Ukihubiri jambo lile lingine mtu yule mwingine hatapendezwa. Muda si muda hakutakuwa na wakati “unaofaa” kwa wahkubiri kuhubiri ujumbe wa aina fulani. Basi tutafanyeje? Je, tutapiga magoti mbele ya msukumo upi? Tutahubiri nini?

Wewe lihubiri Neno. Uhubiri ukweli. Hubiri kile ambacho Mungu amekusukuma kuhubiri. Kamwe usimwogope mwanadamu yejote. Usihofie cheo chake. Usiwaogope wanadamu wale wengine. Wakati mwingine utaona upweke, lakini Mungu atakuwa mwaminifu kwa wajumbe wake na kwa ukweli wake.

—mws